

## **MUHTASARI WA LUGHA WAZI YA SERA YA MSAADA WA KIFEDHA WA HUDUMA YA AFYA**

### **Muhtasari**

Kulingana na dhamira yake ya kuboresha afya ya jumuiya zake, huku msisitizo maalum ukiwekwa kwa watu maskini na wasio na huduma za kutosha, na katika roho ya huduma ya uponyaji ya Yesu, Bon Secours Mercy Health imejitolea kutoa msaada wa kifedha kwa wagonjwa wake. Huu ni muhtasari wa Sera ya Msaada wa Kifedha wa Huduma ya Afya (HFA) ya Bon Secours Mercy.

### **Upatikanaji wa Msaada wa Kifedha**

Ustahiki wa msaada wa kifedha huamuliwa kulingana na uwezo wa mgonjwa au mdhamini wake kuweza kulipa baada ya rasilimali zote zilizopo kutumiwa na mipango yote ya msaada iliyopo kutathminiwa. Msaada wa kifedha unapatikana kwa dharura na huduma nyiningine muhimu za kiafya zinazotolewa na hospitali za Bon Secours Mercy Health (na baadhi ya watoahuduma wengine) kwa wagonjwa wasio na bima na wenye bima isijoitosheleza wanaoishi katika jumuiya zinazohudumiwa na hospitali za Bon Secours Mercy Health, na ambao mapato ya familia zao si zaidi ya mara nne ya Miongozo ya Umasikini ya Shirikisho (FPG).

### **Mahitaji ya Ustahiki**

Msaada wa kifedha kwa kawaida huamuliwa kwa kutumia kiwango kinachobadilika kulingana na jumla ya mapato ya kaya kwa mujibu wa FPG. Watu wanaostahiki msaada wa kifedha chini ya Sera yetu walio na kiwango cha mapato cha 200% ya FPG au chini ya hapo wanapokea huduma bila malipo. Watu wenye kiwango cha mapato kuanzia 201% hadi 300% ya FPG, na 301% hadi 400% ya FPG, kwa mtiririko huo, wanapokea huduma kwa punguzo kulingana na kiwango kinachobadilika, kama ilivyoainishwa katika Sera. Asilimia maalum za mapunguzo kwa ajili ya viwango vya mapato vya 201%-300% ya FPG na 301% hadi 400% ya FPG husashisha kila mwaka kwa kila soko kulingana na mabadiliko katika orodha kuu ya ada.

Hakuna mtu anayestahiki msaada wa kifedha chini ya sera ya HFA atakayetozwa zaidi kwa huduma za dharura au huduma nyininge za matibabu za lazima zaidi ya kile kiasi ambacho kwa kawaida hutozwa kwa watu wenye bima inayoghamia huduma hizo. Ikiwa mtu ana bima inayojitosheliza au mali zinazopatikana kwa ajili ya kulipia huduma, anaweza kuonekana kuwa hastahili msaada wa kifedha. Kwa wagonjwa wasiokuwa na bima ambao hawastahili punguzo lolote la msaada wa kifedha kama ilivyoolezwa katika sera ya HFA, Bon Secours Mercy Health inatoa punguzo la kiotomati (kulipa mwenyewe) kwa bili zao za hospitali. Tafadhali rejelea Sera kamili ya HFA kwa maelezo kamili.

### **Kuhusu Mchakato wa Kutuma Maombi**

Mchakato wa kutuma maombi ya msaada wa kifedha chini ya Sera yetu ya HFA unajumuisha hatua hizi:

- Jaza Fomu ya Maombi ya HFA na ujumuushe hati muhimu zinazohitajika.
  - Tunaangalia mapato yako na ukubwa wa familia ili kubaini kiwango cha msaada unaopatikana kwako. Tunatumia kiwango kinachobadilika, kulingana na FPG ilivoainishwa hapo juu.
  - Tunahitaji kwamba lazima uangalie kwanza ustahiki wa manufaa ya bima ya aina fulani ambayo itaweza kugharamia huduma zako (yaani, fidia ya mfanyakazi, bima ya gari, nk). Tunaweza kukusaidia kukuelekeza kwenye nyenzo zinazofaa.
- Tutawasiliana nawe ili kukuambia ikiwa unastahiki msaada wa kifedha chini ya Sera yetu ya HFA.
- Tunaweza kukusaidia kupanga mpango wa malipo kwa ada au bili zozote zilizosalia ambazo hazigharamiwi chini ya Sera yetu ya HFA.
  - Mpango wa malipo utazingatia hali yako ya kifedha ili kuweka malipo ambayo unaweza kuyamudu.

### **Mahali pa Kupata Taarifa**

Unaweza kupata nakala ya Sera yetu ya HFA na Fomu ya Maombi ya HFA, pamoja na taarifa kuhusu mchakato wa maombi ya msaada wa kifedha: (i) kwa kutembelea tovuti yetu kwenye [www.bsmhealth.org/financial-assistance](http://www.bsmhealth.org/financial-assistance), [www.mercy.com/financial-assistance](http://www.mercy.com/financial-assistance), na [www.fa.bonsecours.com](http://www.fa.bonsecours.com), au (ii) kwa kuwasiliana na Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa za Secours Mercy Health kwa njia ya simu kwa 1-855-732-0138, (iii) kwa kutuma maombi kwa Mercy Health Public Benefits Dept, PO Box 631774, Cincinnati, OH 45263-1774, au (iv) kwa kuwasiliana na washauri wetu wa kifedha ana kwa ana katika maeneo yoyote ya hospitali zetu (tazama Sera Kamili ya HFA ili kupata orodha kamili ya vituo na anwani).

Tunatoa huduma kwa makundi yote makubwa yanayohudumiwa na Bon Secours Mercy Health ambayo yana ufanisi mdogo katika Kiingereza kwa kutafsiri nakala za Sera yetu ya HFA, Fomu ya Maombi, na Muhtasari huu katika lugha kuu zinazozungumzwa na makundi hayo. Tunaweza pia kuchagua kutoa misaada ya tafsiri, miongozo ya tafsiri, au kutoa msaada kupitia matumizi ya wakalimani walio na uwezo wa lugha mbili.